Jiwe la kiroho la kujengea no.50

# Ile Nchi ya ahadi ni kuishi katika Nchi ya Roho Mtakatifu

''Ikawa baada ya kufa kwake Musa mtumishi wa Bwana, Bwana akamwambia Yoshua mwana wa Nuni mtumishi wa Musa, akasema, Musa mtumishi wangu amekufa haya basi ondoka ukavuke mto huu wa Yordani wewe na watu hawa wote mkaende hata nchi niwapayo wana wa Israel, kila mahali litakapo kanyaga nyayo za miguu yenu nimewapa ninyi kama mlivyo mwapia Musa''***(Yoshua 1:1-13)***Hiyo ndiyo ahadi, nchi ya ahadi ni kuishi katika nchi hii ya Roho Mtakatifu. Hiyo ni ahadi ya Mungu kwa kanisa, ni kuishi katika nguvu za Roho Mtakatifu. Hiyo ni dunia nyingine, Hiyo ni nchi nyingine. Inabidi utoke katika hali ambazo ulikuwa katika hizo. Ili utoke uishi katika nchi hii ya ahadi, kuipokea ahadi, kumbuka ile ahadi''Utapokea nguvu kutoka juu baada ya Roho Mtakatifu kuja juu yako''…..hiyo ni ***(Matendo1:8)*** [1]

Kule kutoka kwa pili, alimleta nabii, aliyepakwa mafuta (Yesu Kristo) ambaye alikuwa mwanawake mungu nabii. Musa alisema yeye angekuwa nabii na alikuja na ile nguzo ya moto na akafanya ishara na maajabu. Nabii huyo alisema kwamba anaye niamini mimi kazi ninazozifanya naye atazifanya ***(Yohana 14:12)***

Na mahali hapa amehaidi jambo lile lile katika kutoka katika siku za mwisho na hawezi akabadilisha hilo. Na kwa ushahidi wa Roho na kwa kazi ya Roho tunaona leo ile nguzo kuu ya moto ikitembea miongoni mwetu; na ishara ya na maajabu ya kufufuka kwa Yesu Kristo yakiwaita watu kutoka kwenye madhehebu, kuja uweponi mwa Yesu Kristo kuishi, kwenda kwenye nchi. [2]

Kwa hiyo tunaweza kuwa na shukrani kama wasafiri, kama Ibrahim; tukiwa tumetengwa sisi wenyewe na vita vya dunia.Washirika wetu wote ***(2 Wakoritho 6:14-18).*** Ibrahimu alikuwa msafiri, Mungu ametutenga sisi kutoka kwenye madhehebu kwenye dini zote zilizokufa. Ninazungumza kwa Taifa lote sasa kanuni zote zilizokufa. Na nini tena?, ametutenga sisi na akatufungulia sisi nchi mpya ujumbe mpya kwa siku hii ya leo. Pentekoste imekaukiwa na imekufa kama vile Luther, Wesley na wengine wote.sio zaidi ya kundi la makanisa liliojiunga pamoja watu wazuri wako pale. Lakini inabidi watoke humo. [3]

Sasa tumeona aina zote za miamsho mikubwa na kupiga kelele na kumsifu mungu; Yote ni mazuri tumenena kwa lugha na kutoa unabii wa yote.Tumeona hayo yote hayo ni mazuri yanaenda pamoja na hilo .Lakini kumbuka jambo la mwisho ni uwepo wake wa kiungu lile neno lenyewe,yeye ni neno kile kichwa,lile neno linakuja katika mwili. Unaona, halafu lile neno ***(Waebrania 4:12-13)*** ulisema ''Neno la mungu lina nguvu ni kali kuliko upanga wao wowote; ukatao kiwili tena lachoma hata kuzigawanya Roho na nafsi na viungo na mafuta yaliyomo ndani tena jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo''Sasa chukua hilo andiko na ulifuatilie tangu mwanzo katika manabii na uendelee mpaka Yesu Kristo,Na uone kama siyo jambo hilo. Ni jambo hilohilo kwamba anajulikana kama masihi. Siyo kwamba ni mtu Fulani hapa ambaye ni masihi, Ni Roho ambaye ndiye masihi, Kristo na Roho Mtakatifu ni kitu

kilekile, kwahiyo kiko hapa sasa kikitenda kazi katika mwili kuunda mwili uwe tayari kwa ile neema ya kunyakuliwa. [4]

Ni wangapi wanajua kuwa kuna tofauti kati ya kule kuonekana kwa kristo na kule kuja kwa Kristo? Ni maneno mawili tofauti,sasa hivi ni wakati wa kuonekana ***(2 Timotheo 4:8)*** kule kuja kwake kutakuwa karibuni sasa hivi ni wakati wa kuonekana miongoni mwetu akizitenda kazi alizozitenda katika kanisa lake. Sasa wewe ni sehemu ya hilo kanisa lake na kwa neema unaamini kwamba mimi ni sehemu ya hilo kanisa sasa mimi siyo mhubiri,unajua mimi siyo, mimi sina Elimu ya kufanya hivyo. Wakati mwingine najiona asiyependa kusimama miongoni mwa watu wa mungu. Walioitwa kwa ofisi hiyo, kuna mitume, kuna manabii kuna walimu, kuna wachungaji na wainjiristi ***(Waefeso 4:11-12),***siyo wote ni mitume,si wote ni walimu , sio wote ni wainjiristi ***(1 Wakoritho12:28-30)*** lakini huduma yangu ni tofauti sana naya mchungaji au mwalimu, mimi siyo , na kama nikisema kitu kimakosa ndugu mnisamehe mimi. Simaanishi hivyo.Lakini hii ndio huduma yangu kumtangaza yeye kwamba yuko hapa ***(Ufunuo 10:1-7)*** [5]

Baada Yakobo kushikana miereka usiku kucha katika kutubu dhambi zake unakumbuka mahali alipokuwa palitoa panieli hiyo ni ***(Mwanzo 32:22-32)*** Neno Panieli katika Kiebrania maana yake ni’’uso wa Mungu Mkuu’’.Yakobo Yule mdanganyifu jina lake lilikua Yakobo lenye maana’’ mdanganyifu’’***(Mwanzo 27)*** katika maisha yake yote alikuwa anakimbia mbali na Mungu. Lakini alipokuwa katika uwepo wa Mungu kule Penile. Katika uso wa Mungu hakutaka kumuachia yeye.Mungu tunahitaji watu wengi aina ya yakobo.Alimshikilia mungu mahali pale pa uso wa mungu,akiwapo uweponi pa mungu,akimshikilia mpaka jua likapanda juu. Mungu akasema’’ niache niende maana jua linapanda juu’’Alikaa uweponi pa uso wa mungu mpaka jua limepanda,lakini aliondoka akiwa amehesabiwa haki na kuokolewa,

Ilikuwa ni kitu kikubwa sana, kujua kwamba alishikana mieleka mpaka akashinda. Nikwamba Yeye alioteshwa ishara za Mungu, aliota ndoto juu ya mungu, lakini hapa ni mara ya kwanza kuwa mbele ya uso wa Mungu,Akiwa uweponi pa Mungu .fikiria juu hilo,Marafiki? Kuwa katika uwepo wa mungu, Mwanadamu anakuwa mtu asiyebadilishwa.Yakobo alibadilishwa sasa anaweza akatembea na Mungu, ndio Yeye alikuwa ni mtu tofauti ya vile ambavyo ameenda pale.Vitu sasa vilikuwa vimekwisha, ndio Bwana ndipo akaanza kujenga madhabahu.Hakuwa amewazoea kujenga madhabahu, unajuwa,lakini, nakuambia wewe unapokuja uweponi pa Mungu unataka kujenga madhabahu sehemu Fulani. Unataka kutafuta mahali Fulani ambapo unaweza ukaomba, yeye alijenga madhabahu, alikuwa amesafika na Mungu alikuwa ameshinda.

Katika ***(Zaburi 16:8)*** Daudi alisema “Nimemuweka bwana mbele yangu daima” hilo ni jambo zuri la kufanya, kusudi usiweze kuchanganyikiwa juu ya hilo, alitaka uwe na ufahamu juu ya uwepo wa Bwana, kwa hiyo Daudi alisema “nimemuweka Bwana siku zote mbele za uso wangu, sasa mimi Daudi nimemuweka Bwana mbele za uso wangu, siku zote ili kuwa na ufahamu juu ya uwepo wa Mungu,je hilo halitakuwa ni somo zuri, kwa sisi wote hapa kumuweka Bwana mbele ya nyuso zetu ili tuwe na ufahamu wa uwepo wake, muweke Yeye kuwa wa kwanza mbele zako.Kwa nini? Hapo sasa hutaweza kutenda dhambi. Unapowaza sasa wakati wote upo uweponi pa Mungu ***(Zaburi 119:11)*** unapotambua kwamba Mungu amekuzunguka,utajali sana kile unachosema na utakuwa makini na kile unachosema.Mtu anapofikiri Mungu ameondoka, atalaani, atashikwa na tama za wanawake,ataiba, atadanganya, atasema uongo, atafanya kitu chochote anachofikiri kwamba Mungu hamuoni yeye, lakini mlete Yeye katika uwepo wa Mungu, ataacha hilo sasa. Unaona? Na Daudi alisema “nimemuweka Bwana mbele zangu daima) hilo ni jambo zuri, sio ajabu Mungu alisema Daudi ana moyo

unaofanana na wake, mtu atafanya kitu chochote anapofikiri, kwamba Mungu hayupo karibu. Je! Uliwahi kumuona mwenye dhambi? Kama mtu atasimama mbele yake, ataacha kulaani kwake, kama ana chembe yoyote ya heshima, unaona? Hatasema ile mizaha michafu ambayo angeisema. Unaona, ataacha hayo kwa sababu Mungu anaishi katika maskani ya watu wake. ***(Efeso 2:20-22)*** Tunapokuja uweponi mwake, hatuwi vile tulivyo tena, angalia kule nyuma katika nyakati zile, katika mwenendo wa maisha ya mwnadamu, mwangalie Abrahamu, unasema "vema, maisha yaliyobadilishwa nikiwa wahudumu tu" Oh hapana maisha yaliyobadilishwa ni kwa kila mtu. [6] Lakini angalia hapa nataka ujaribu kufanya jambo hili, ondoa ile mbegu ya hitilafu mbali na wewe sasa, na uamini neno la Mungu ambalo limefanyika hai, katika miili yetu wenyewe. Hilo linaonyesha uwepo wa Mungu [7]

Sasa kama utaangalia hapa ile safari yao kule jangwani ndipo mahali Israeli walifanya kosa kubwa sana mpaka Kalvari ilikuwa pale katika ***(Kutoka 19)*** walikubali sheria badala ya neema, walikuwa na neema, walikuwa na nabii, walikuwa na mwanakondoo wa sadaka, walikuwa na ukombozi, walikuwa wamevushwa kupitia bahari ya Shamu, walikuwa wameponywa magonjwa yao ***(Hesabu 21:4-9),*** walikuwa na maji yaliyotoka kwake kwenye mwamba uliopigwa
(1 wakorintho 10:1-4, mwanzo 17:16)

Walikuwa na mana iliyotoka mbinguni (kutoka 16) kila kitu walichokuwa wanakihitaji walipewa, lakini bado walitaka kitu kingine, sasa hiyo ni mfano mkamilifu wa Efeso yetu ya leo, hiyo ni sahihi kabisa, tumetoka chini ya Martin Luther, tumepitia wakati wa utakaso, chini ya Mesodist na tumekuwa katika wakati wa kurudishiwa, chini ya Pentekoste, hiyo ni sawa kabisa, kama ilivyokuwa katika safari. Ile ya jangwani.
Mungu alipotutoa nje tulifanya vizuri sana lakini tulifanya nini? Tulitaka kuwa kama wengine wote lakini tunaona kwamba neema ndio kitu pekee kinachotuvusha sio sheria
***(Waefeso 2:8-9, Warumi 3:20-21)***

Yoshua hapani mfano wa huduma siku za mwisho.Sasa kumbuka hizi hatua tatu za safari zote zilikoma, kwanza ni sheria na kila kitu ilibidi kikome ili Joshua…… Na Yoshua ni neno lile lile sawa na Yesu "Yehova ni mwokozi" hiyo iliwachukua wao kutoka jangwani mpaka nchi ya ahadi. Sitaki niwe asiyekubaliana na hawa wa somi, likini wengi wanafikilia kwamba nchi ya ahadi iliwakilisha Mbinguni. Haingeweza kuwakilisha Mbinguni, Haingeweza kwa sababu kulikua na vita na matatizo na mambo ya kusumbua na kila kitu katika nchi ahadi? Haiwakilishi ile nchi ya ahadi. [8]

Inakuwaje tunaweza kuona ishara kuu na maajabu yakifanywa na watu wengine, vipi kuhusu Sisi? Inatupasa kutoweka katika mazingira ya kutaharuki kwamba sisi tumemaanisha mbele za Mungu, Zile ishara za kuja kwake inapaswa kulileta hili kusanyiko lote wakati hili tumelisoma katika neno. Roho Mtakatifu ametuambia sisi "nenda mahali fulani kitu hiki na kile kitatokea" hakutuambia hasa ni kitu gani lakini kinatokea.Tunaenda pale, vinatokea vilevile tulivyoambiwa, magazeti yanakiandika, majarida yanakichukua, wanaonesha picha zake. Wanakuja nyuma hapa na kuona hizi siri kuu, zilizofichwa katika Biblia zikifunguliwa kwetu katika uwanja mpya hatujawahi kufahamu kabla, na vinaungana vikamilifu na kule kuja kwa bwana Yesu
***(Mathayo 13:10-17),*** sasa pale mwishoni mwa ujumbe angalia yale matendo ya Roho Mtakatifu mkuu, akija hapa akionekana machoni pa watu hata picha zake zikichukuliwa, angalia vile inavyofanya kazi nakuonyesha sio mwanadamu, sio mhubiri tu, sio kusanyiko Fulani, ni Roho

mtakatifu akonyesha mambo yale yale aliyoyafanya alipokuwa ndani ya mwili wa Yesu Kristo, na sasa yako ndani ya mwili wa bibi arusi, inapaswa kutuingiza mahali pa mumtafuta Mungu kwa moyo wote [9]

Ile ndoto ya ndugu Junior Jackson inaelezea kile kinachotokea katika mvuto wa tatu, alimuambia ndugu Branham " nimeota kwamba kulikuwa na mlima mkubwa, kama kule nje kwenye mashamba ambako kuna majani ya bluu au kulikuwa na kitu Fulani, juu kule kwenye kilele cha huu mlima ambako maji yalikuwa yameosha udongo wake, kulikuwa na jiwe kule juu yam lima, kama juu ya mlima ilikuwa ni jiwe hakuna majani ambapo maji yalioshwa yameondoa baadhi ya maandiko kwenye lile jiwe nawe ulikuwa umesimama pale ukitafsiri na kuona kila kilicho kwenye jiwe na ulikuwa umesimama pale na kutafsiri na kutusomea kilichoandikwa kwenye jiwe" Na akasema " sisi sote" na hapa aliliweka hivi, alisema " ndugu Georgia na kutoka sehemu mbalimbali, tulikuwa wote tumesimama sehemu moja, tulikuw tukikusikiliza wewe ukitafsiri yale maandiko ya kisiri yaliyokuwa kwenye hili jiwe katika mlima." Na akasema " ulichukua kitu kama kutoka hewani, kitunkama mtambo wa kupigia" ni hivyo ndugu "kitu Fulani kama mtambo wa kuvunjia ukiwa mkali sana" na akasema " jinsi ulivyofany siwezi kuelewa" na akasema "ulipiga ile sehemu ya juu ya mlima na ukafungua kile kifuniko chake ukakiondoa. Kilikuwa katika umo la piramidi nawe ulipiga pale juu yake"

Sasa hiyo ilikuwa miezi na miezi kabla ya ujumbe ule wa piramidi haujahubiriwa, naye akasema "chini yake kulikuwa na jiwe jeupe" na ulisema " jua au nuru kamwe haitaangaza juu yake hapo mwanzo. Angalieni hili" **(Waefeso 1:15-18)**

Na hiyo ni sawa kwa sababu katika kuumba dunia, dunia iliumbwa kabla ya kuwepo nuru, sisi sote tunafahamu hilo, Mungu akatembea juu ya maji, na hapo mwanzo akazungumza kuwepo nuru na ni wazi kwamba tangu asili, katika kule kuumbwa kwa mawe, nuru haijaangaza kwenye yale mawe kule ndani. Na akasema "angalia hili, nuru haijakuja kwenye hili hapo kabla na wote walipokuja kuangalia nikawaamba waangalie hilo na wote wakaja kuangalia pale ndani, naye akasema wakati walipokuwa wakiangalia pale, akaangalia pembeni ya macho yake. Naamini ilikuwa hivyo, na akaniangalia mimi, nikasogea pembeni nikaanza kueleke magharibi kule ambapo jua lilikuwa linazamia, nikaenda juu ya mlima, kwenda chini yam lima, nikazidi kuwa mdogo na kuwa mdogo mpaka nikawa sionekani, nae akasema nilipofanya hivyo akasema "hapo sasa ndugu wakageuka na kuangalia huku na huku wakasema je? Ametoweka?Amenda wapi? "Akasema wengine wamechukua njia hii na wengine njia nyingine'' lakini wachache sana walikaa na kuanglia kwenye kile nilichowaambia wafanye. Sasa angalia tafsiri ya hii ndoto ambayo nilikuwa sijambwambia hata kitu kimoja, au hata hizi nyingine, sijamuambia mtu yoyote lakini nikasema "ndiyo" na moyo wangu ukitetemeka nilikuwa ninaangalia sasa yale maandiko ya kisiri….. subiri nitaacha hili kwa muda kidogo. [10]

Sikilizeni ninachowaambia, sikiliza kwa karibu, angalia nyuma kule, jipime mwenyewe kwa neno uone uko mahali gani ninyi wanawake mlio na nywele fupi, ziacheni zikue, kama mnavaa kaptula zivue fanya kama mwanamke, ninyi wanaume ambao mnavuta sigara, mnaenda kwenye maholi ya kuogelea, acheni hilo, sijali unafikiri nini kama unashikilia lile dhehebu na kusema "hiki ndicho" ,"na hiki ndicho" afadhali uache rudi nyuma liangalie hilo na neno inabidi tuishi kila kitu na neno,tunapaswa tunapaswa kuishi juu ya haya mambo ya nywele Fupi, na mambo yote ya wakati huu sasa, tuko kwenye kitu kingine,kwamba Mungu anafunua siri zote zilizofichika kabla ya kuwekwa msingi wa dunia, ***(Ufunuo 10)*** na hawa walio tii haya mambo

wataweza kuelewa na haya mambo mengine ***(Isaya 1:19)*** kama hawakutii, itaruka juu ya vichwa vyao kwa kadiri mashariki ilivyo mbali na magharibi. [11]

Na Mungu alipowapa wa Israeli nchi ya ahadi walipokuwa bado Misri ilibidi wapiganie nchi ya nchi. Mungu alimwambia Joshua " kila mahali mtakapokanyaga kwa nyayo za miguu yenu nimewapa ninyi kumiliki" ***(Joshua 1:3)*** kwa hiyo nyayo za miguu "ni kumiliki" watu wengine wanaweza wakafika pembeni kabisa mwa ile nchi, wengine wanaweza wakachukua upanga ukatao kuwili, na kukata katika njia yao wafilisti na waamani mpaka wakachuku sehemu yote hivyo ndivyo tupasavyo kufanya, kila ahadi ni kwa ajili yake, wayo wa mguu ni kumiliki, tembea na uichukue Mungu amtupa hiyo, hiyo ni ahadi na hiyo ni kweli na hiyo ni kwa ajili yetu. [12]

Analifanya neno lake lijulikane kwa watu? Sasa angalia hekima ya Mungu akijua kwamba kutakuwa na wasioamini, na jinsi kwamba hao watakuwa wasioamini, na jinsi kwamba wao watakuwa wasioamini yeye kwa kujua kimbele ***(Warumi 8:29-30)*** alichagua kimbele mbegu ya kila wakati ambao wataliamini hilo, sasa kama utaangalia pale, kila wakati anaenda pale na neno lake, kila kitu kwa wakati wake, hakuna kinachomzuia Mungu, anaendelea pale na kila mshale unapotembea uko sawasawa kabisa, wakati mwingine tunawaza kwamba haitafanya kazi vizuri, lakini usiwe na wasiwasi, saa yake imerekebishwa kikamilifu kabisa, subiri kwa dakika yeye amesema " mimi saa yangu inazunguka kikamilifu kabisa inabidi nikuweke wewe katika msingi uleule ambao nilimuweka mtu wa kwanza, katika siku zile, nimweke katika msingi uleule wa Martin Luther na katika msingi uleule wa Wesley" kwa sanbabu unaona haikujulikana wakati ule kama sasa , na tunapopata maandiko mengi sasa zaidi ya wakati ule na adui anapokuja kama mafuriko, Roho wa Mungu anainua kiwango cha kumpinga. ***(Isaya 59:19)*** unaona na sasa leo tuna maarufa zaidi, tuna uelewa zaidi ***(Daniel 12:4,9-11)*** kwa hiyo mito ya kuto kuamini inatitirika kwa nguvu sana, lakini Mungu anainua kiwango cha kuipinga hiyo hali, sababu inayofanya kwamba alichagua kimbele, haya mambo yatokee, aliwaambia manabii wake kimbele yake ambayo itatokea, na wenye haki wanapoona haya mambo yanathibitishwa, hapo sasa wanajua ni kweli. [13]

Sasa kule kumalizia ni kweli kwamba Mungu anashughulika na waIsraeli tu wanapokuwa kwenye nchi yao, wakati Ibrahimu alipoacha nchi ya nyumbani anaenda Misri, kulitokea nini? Alitembea mbali na mapenzi ya Mungu, na kamwe hakubarikiwa mpaka aliporudi kwenye nchi ya nyumbani ***(Mwanzo 12:9-20, 13:1-4)***

Mungu hakushughulika naye hata kwa ono moja wala kitu kingine chochote mpaka aliporudi kwenye nchi ya nyumbani. Angalia Waisraeli walipotumwa kwenda Misri, miaka minne hakukuwa na miujiza hata mmoja, hakukuwa na ishara hata moja, wala kitu chochote kilichotoke miongoni mwao, kilichorekodiwa katika historia ya kitabu. Na Mungu kamwe hakushughulika na WaIsraeli mpaka waliporudi nchi ya nyumbani, nisikieni mimi HII ASEMA BWANA Mungu hatashughulika na kanisa lake mpaka lirudi nchi ya nyumbani ujumbe wa saa hii, rudini kwenye lile neno la asili, achilieni mbali umethodith wenu, ubaptist wenu uprestheiterian na ya kipentekoste na mawazo ya kipentekoste na kiasemblisi na kiumoja na kiutatu na kiutano.

Chochote iwaacho kanisa la Mungu wapirigrimuhorines kanisa la Kristo yote haya ni vikundi vya mpinga kristo na tambua kwamba hili linaenda duniani kote, yote yamepotoka, yote ni ya kishetani…kuna watu wa Mungu katika kila moja la haya siyo ya Mungu na Mungu hatayabariki, kamwe hajafanya hivyo, kamwe hajabariki wa Israeli mpaka wamekuja kwenye nchi ya ahadi, na walipokuja kwenye nchi ya ahadi ishara na miujiza vilianza kutokea. [14]

Kama vile Musa alivyotoa taifa kutoka ndani ya taifa, Kristo leo anaita kanisa kutoka ndani ya kanisa unaona? Jambo lilelile kwa mfano akiwachukua wao kwenye ile nchi ya utukufu, nchi ya milele nchi ya ahadi. [15]

Sasa na tuombe Mungu atupe dawa ya macho ya Roho mtakatifu na kupaka katika macho yetu ili kufungua macho yetu,Bwana Mungu naweza kuhubiri mpaka nipoteze pumzi yangu, na wahuduma wengi wafanye jambo hilo hilo, tunaweza tukasimama hapahapa na haijalishi tufanye nini, hatuwei kwenda popote bila ya wewe kutuonesha sisi njia ya kuendea, tunahitaji macho ya ki Roho, mruhusu Roho Mtakatifu, Bwana fungua macho yetu ***(Matendo 26:18)*** fungua uelewa wetu tuoneshe sisi uwepo wake, ili yuweze kuona ahadi zake tena na tena, kupitia kwenye maandiko, kupitia kwenye Biblia tumeyaleta hayo ambayo umeyaahidi haya mambo, na tunaishi hapa tukiyaona hayo, hapa mbele yetu, mbele ya macho yetu, tupe hayo Bwana katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo. Amen. [16]

## Nukuu za kingereza


[1] Maswali na majibu (61-1015m) Aya 70
[2] Kule kutoka kwa tatu (63-0630m) Aya 265-266)
[3] Muungano usio onekana wabibi ANSI (65-1125) Aya194 -195
[4] Jeho ya yire part1 (64-0402) Aya 194-196.
[5] Kutoka ile saa (62-0713) Aya 102.
[6] Katika uwepo wake (62-0909e) aya
[7] Ile mbegu ya hitilafu (65-0118) Aya 127
[8] Kile kitenawili (65-0117) aya 79-82
[9] Kutafuta kwa moyo wote (63-0901E) Aya 53-54
[10]Je mabwana hii ndio ishara ya mwisho (62-1230E) Aya 126 -134
[11] Maswali na majibu katika mihuri (63-0324m) A213-216
[12]Tunataka kumuona Yesu (62-0704) Aya71
[13]Kuthibitisha neno lake ( 64 -0816)Aya72-74
[14]Maagizo ya Gablieli kwa Danieli (61-o730m) Aya 130-137
[15]Uongozi (65-1207) Aya 141
[16]Mlango wa kwenda moyoni (59-1128) Aya51



*Jiwe la kiroho la kujengea na 183 kutoka Neno lililofunuliwa la saa hii. Iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69-D– 75328 Schomberg Germany Simu (+49) 7235 - 7613. Fax (+49) 7235 3306.*


*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia, zile mbegu zitaingizwa magazetini na vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu ya Mungu iliyochaguliwa kimbele imesikia hilo (Ndg. Branham katika mwenendo na mafundisho uk 724)*


*Kwa nakala zaidi za kiingereza na kiswahili. Andika kwa: Charles E. Y. Kanju*

*Box 553 Korogwe - Tanga*

*E-mail: Chaelika@livel.com*

*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*